Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 4, Issue 1

28th Dhul-Qa'dah 1431

5th November, 2010

SIKU ZILIZOBARIKIWA ZA DHUL-HIJJAH

Mtayarishi: Sheikh Muhammad al-Jibaaly

Kutokamana na Ukarimu wake mkubwa usio na kifani, Allaah (سبحانه وتعالى) amewajaalia waja wake, walio mahujaji na wakaazi, idadi ya masiku yaliyobarikiwa. Masiku hayo ni yale kumi na tatu ya mwanzo ya mwezi wa kiislamu ya Dhul-Hijja. Katika yafuatayo tutagusia baadhi za Sunnah kuhusu siku hizo tukitarajia kwa hayo kujiandaa na kuwa na hima ili tufanye yalio bora.

SIKU KUMI ZA MWANZO WA DHUL-HIJJA—Fadhila Zake

Siku kumi za mwanzo wa Dhul-Hijja zina fadhila maalumu na umuhimu katika Uislamu. Nayo ni masiku yaliyo bora katika mwaka mzima. Amali njema zinapendwa zaidi na Allaah (سبحانه وتعالى) na kwahivyo zina malipo makubwa zaidi kwenye siku hizo. Jabir Bin 'Abdillah (رضي الله عنه) akapokea kutoka kwa Mtume صلى (الله عليه وسلم) kuwa amesema: *"Siku zilotukufu ulimwenguni ni siku kumi."*
Na akapokea Ibn Abbas (رضي الله عنه) kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Hakuna masiku ambayo amali njema zinapendwa zaidi na Allaah kama masiku haya (kumi)."*
Kisha nae Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaulizwa: "Hata pia Jihad kwa njia ya Allaah?" akajibu: *"Hata pia Jihad kwa njia ya Allaah isipokuwa kwa yule alokwenda (Jihad) kwa nafsi yake na mali yake na asirudi na kitu (akapoteza hayo yote) kwa ajili ya Allaah."*

Tufanyeje Katika Siku Hizi:

Kama ilivyo-onyesha kwenye Hadithi hiyo ya mwisho, amali zote njema ni zenye kupendwa na Allaah katika siku hizo. Ma-Salaf wameifahamu vizuri sana; ikapokewa yakwamba wakati mmoja katika siku hizi kumi zilipoanza, Sa'id Bin Jubayr alijitahidi kupita kiasi (kufanya Ibada) mpaka akafika kiwango cha kujikalifisha.
Hasa zaidi, kufunga na kufanya dhikr (kumtaja na kumkumbuka Allaah) yanatakikaniwa kufanywa zaidi katika siku hizi.

Dhikr:

Ibn Umar na Abu Huraira (رضي الله عنه) walikuwa wakienda sokoni kwenye hizi siku kumi wakifanya takbir. Na watu walikuwa wakifuata mfano wao nao wakisema takbir pia. Hii yaonyesha utwiifu wao kwa amri ya Mtume صلى الله (عليه وسلم) kama ilivyopokewa na Ibn Umar (رضي الله عنه): *"Hakuna masiku yaliyo matukufu mbele ya Allaah, na ambayo amali njema zinapendwa zaidi na Yeye, zaidi ya hizi siku kumi, kwahivyo sema (wakati huo) kwa wingi, tahlil (La ilaha illallah – hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki illa Allaah), takbir (Allahu Akbar – Allaah ni Mkubwa) na tahmid (Al-hamdu lillah – Sifa zote na shukurani ni za Allaah).*
Na katika tafsir (ufafanuzi) ya Aya **"... na kulitaja jina la Allaah (kwa wingi) katika siku zinazojulikana"**,[Al-Hajj 22:28] Ibn Abbas akasema: **"Siku hizi zinazojulikana ni siku kumi (za Dhul-Hijjah)."**

Kufunga:

Mmoja katika wake za Mtume صلى الله عليه (وسلم) amesema: "Mtume wa Allaah صلى (الله عليه وسلم) alikuwa akifunga siku tisa za mwanzo za Dhul-Hijjah, siku ya Ashura na siku tatu za killa mwezi."
Walaakin kufunga siku zote hizo sio wajib wala sio sunnah iliyo thabiti ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwahi kuikosa. Akasema 'Aaisha (رضي الله عنها), "Sikuwahi kumuona Mtume (صلى الله عليه وسلم) akifunga hizo siku kumi."

Siku Ya Arafa:

Siku ya tisa ya mwezi wa Dhul-Hijjah inaitwa siku ya Arafa kwa sababu

Yaliyomo

Siku Zilizobarikiwa za Dhul-Hijjah 1 - 2

Ibada Ya Kuchinja 2 - 4

Mahujaji huja kusimama kwa ibada kwenye mlima wa Arafa siku hiyo. Hiyo ni siku bora ya masiku yote ya mwaka mzima. Abu Qataada akapokea Hadithi kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa amesema: *"Saumu ya siku ya Arafa hufidia madhambi ya miaka miwili: mwaka ulopita na mwaka ujao. Na saumu ya siku ya 'Ashura hufidia dhambi za mwaka ulopita."*
Na 'Aaisha (رضي الله عنها) akatuahadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Hakuna siku ambayo Allaah huwaacha watu huru na moto kama siku ya Arafa. Huja karibu (ya wale waliosimama Arafa) na kisha Akanadi mbele ya malaika Wake Akisema: 'Ni kitu gani wanachotaka hawa watu.'"*

Siku Ya Adh-ha:

Tarehe ya kumi ya Dhul-Hijja ndiyo 'Idd ul-Adh-ha au siku ya An-Nahr (kuchinja). Siku hii inaashiria kukamilika kwa kanuni za ibada za mahujaji na kuadhimisha Ukarimu wa Allaah (سبحانه وتعالى) juu ya Mtume wake Ibrahim (عليه السلام) alipomruzuku kondoo dume amchinje kama kikombozi cha mwanae Ismail (عليه السلام).
Siku hii ni mojawapo ya siku kuu mbili kubwa ambazo Allaah (سبحانه وتعالى) amewaridhia waislamu. Anas (رضي الله عنه) akatuhadithia yakwamba siku moja Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwaona watu wa Ansar wakisherehekea siku fulani. Akaiulizia siku hiyo na akaelezewa, "Hii ni mojawapo ya siku mbili ambazo tulizokuwa tukisherehekea wakati wa jaahiliyya na mpaka leo twaendelea nayo." Nae akawajibu: *"Kwa hakika Allaah (سبحانه وتعالى) amewabadilishia nyinyi siku mbili bora: Siku ya Al-fitr na siku ya Al-adh-*

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

...DHUL-HIJJAH

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

ha."
Vile vile, Swahaba 'Uqbah Bin 'Amir (رضي الله عنه) akaipokea Hadith kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa amesema: *"Siku ya Al-Fitr, siku ya an-Nahr na siku ya Tashriq ni siku zetu za 'Idd sisi waislamu. Hizo ni siku za kula na kunywa."*
Siku ya an-Nahr ni siku tukufu baada ya 'Arafa. 'Abdullah Bin Qart (رضي الله عنه) amepokea kutoka kwa Mtume صلى الله عليه (وسلم) kwamba amesema: *"Siku zilotukufu mbele ya Allaah (سبحانه وتعالى) ni siku ya an-Nahr, kisha siku ya al-Qarr(makao)"*[Hii ni siku ya kumi na moja ya Dhul-Hijja, ambayo mahujaji huweko kwenye "makao" hapo Mina]
Hiyo ndiyo siku kuu ya Hajj iliyotajwa kwenye Qur'an[At-Tawba 9:3] Ikathibitishwa siku hiyo na Hadith ilopokewa na 'Ali (رضي الله عنه): *"Siku kuu ya Hajj ni ile siku ya kuchinja."*

Siku Tatu Za Tashriq:

Siku za tashriq [Maana ya Tashriq ni kukausha nyama, na siku hizo tatu zikaitwa hivyo kwa sababu, hapo watu kawaida hukata nyama za vichinjo vyao na kuzikausha kwenye jua] ni zile siku tatu zinazofuata *'Idd-ul-Adh-ha*. Katika siku hizo mahujaji hukamilisha nguzo zao za hijja. Waislamu wakaendelea na sherehe zao za 'Idd na wamekatazwa kufunga. Kwenye riwaya nyengine ya Hadith ya 'Uqbah Bin 'Amir (رضي الله عنه) iliyopita, ameeleza kuwa Mtume صلى الله (عليه وسلم) amesema: *"Siku ya Arafa, siku ya Kuchinja na siku ya Tashriq ndiyo 'Idd yetu (waislamu). Nazo ni siku za kula na kunywa."*
Akasema 'Amr Bin al-'Aas (رضي الله عنه) kuhusu siku za Tashriq: "Hizi ni siku ambazo Mtume (صلى الله عليه وسلم) alizotuamrisha tule na akatukataza kufunga." Nubayshah al-Huthali (رضي الله عنه) akapokea kutoka kwa Mtume صلى الله (عليه وسلم) kuwa amesema: **"Siku za Tashriq ni siku za kula, kunywa na kumtaja Allaah (سبحانه وتعالى) "**
Na Abu Huraira (رضي الله عنه) akapokea kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuwa amesema: *"Siku za Mina ni siku za kula na kunywa."*

IBADA YA KUCHINJA

Mtayarishi: Sheikh Muhammad al-Jibaaly

UTANGULIZI

Miongoni mwa vitendo muhimu vya ibada katika siku ya 'Idd ul-Adha pamoja na siku tatu zinazofuata ni Udh-hiyah (uchinjaji). Na hili neno udh-hiyah au dahiyyah limekusudiwa kwa Ngamia na Ng'ombe (kondoo na mbuzi) wanaochinjwa ifikapo siku ya an-Nahr na siku za Tashriq kama sadaqa kwa ajili ya MwenyeziMungu (سبحانه وتعالى). Vile vile neno hili limetokamana na dahwah (katikati ya mchana), mwanzoni mwa nyakati ambapo jambo hilo linapotekelezwa.

Umuhimu Na Fadhila Zake

Allaah (سبحانه وتعالى) ametaja kitendo cha uchinjaji pamoja na ibada ya mwanzo na bora zaidi katika uislamu: Swala. Hii ni kuonyesha kiwango kikubwa cha umuhimu wake. Kwani alimuamrisha mtume wake (صلى الله عليه وسلم) achinje wanyama hao kwa kusema: **"...Basi swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (vichinjo vyako..."** [al-Kawthar 108:2]
Na Allaah (سبحانه وتعالى) akasema: **"Sema: 'Hakika swala yangu na kuchinja kwangu, na uzima wangu, na kufa kwangu ni kwa Allaah, Muumba wa walimwengu wote. Hana mshirika; na haya ndiyo niliyoamrishwa na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha.'"** [Al-An'aam 6:162-163]

Hukumu Yake

Rai ya wanavyuoni wa ki-islamu ni kwamba Udh-hiyah ni Sunna muhimu, na ni ibada iliyohimizwa katika sheria ya Allaah (سبحانه وتعالى). Hata hivyo, imekuja ikhtilafu baina yao iwapo jambo hilo ni nafl (kitendo kisichokuwa wajib) au wajib (kitendo cha lazima) kwa wale wenye uwezo. Rai ya kwamba ni wajib ndiyo iliyo kwenye usawa kutokamana na ushahidi ufuatao.
Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwazuiya watu wenye uwezo walioamuwa kutochinja kuja kuhudhuriya swala ya 'Idd pamoja nae. Ni wazi ya kwamba, hangeliwazuiya kuja kuswali na yeye isipokuwa wameliwacha jambo la wajib. Ikapokewa hadithi kutoka kwa Abu Huraira (رضي الله عنه), akasema Mtume (صلى الله عليه وسلم): *"Kwa yule mwenye uwezo wa kuchinja na asichinje, basi asiukurubie musalla wetu (Kwa swala ya 'Idd)."*Kuhusu hadithi hii, Imam ash-Shawkani akasema: "Kumkataza mtu kuhudhuria musalla kwa sababu ya kuwacha kuchinja haliyakuwa alikuwa na uwezo inaonyesha ya kwamba ameacha jambo la wajib. Kwahivyo niwazi yakwamba Swala yake haina maana bila ya wajibu huo."[Tazama Naylul Awtwaar]
Ikapokewa hadithi na swahaba Jundub Bin 'Abdallaah al-Bujali (رضي الله عنه) yakwamba alishuhudia Adh-ha pamoja na Mtume Muhammad صلى الله (عليه وسلم) Pindi tu alipomaliza kuswali swala ya 'Idd, aliona yakwamba tayari watu wameshachinja kabla hata hajamaliza swala, kwahivyo akasema: *'Ama kwa wale waliochinja kabla hatujaswali basi nawachinje tena badala yake. Na wale ambao hawajachinja wafanye hivyo sasa, kwa jina la Allaah."*
Amri hii kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) yaonyesha ule uwajibu wa kuchinja. Vile vile swahaba Makhnaf Bin Sulaym akaipokea kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwamba amesema: *"Kila nyumba inawapasa kuchinja kila mwaka..."*
Kama tulivyotaja hapo mbeleni, baadhi ya wanavyuoni wanamsimamo yakwamba kuchinja si jambo lililohimizwa kwa wale wenye uwezo. Na misingi ya rai hiyo imetokamana na maswahaba, wakiwemo Abu Bakra

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

SHEIKH UNIFORMS

DEALERS IN UNIFORMS AND GENERAL SUPPLIES

→ SCHOOL UNIFORMS
→ SAFETY WEAR
→ CORPORATE WEAR
→ INDUSTRIAL UNIFORMS
→ PROMOTIONAL ITEMS
→ EMBROIDERY/PRINTING

ENQUIRIES:
Main Office
P.O. BOX 2192, MOI AVENUE,
KARIMI HSE, GROUND FLOOR(NEXT TO TUSKS)
TEL:041 2316749/041 2315075, MSA, KENYA
MOBILE: 0724 173362/ 0733 768250
WEBSITE: www.sheikhuniform.com
EMAIL: sheikhuniforms@yahoo.com

WORKSHOP
BAJUNI ROAD PATEL SAMAJ,
TEL: 041 2316749
MOBILE: 0727 284484

OTHER BRANCH(OPENING SOON)
MWEMBE TAYARI ROAD
OPP. GURU NANAK PRIMARY SCHOOL

na Umar (رضي الله عنه), ambao hawakuitakidi kuwa ni wajib. Vile vile wakaitegemea hadithi ya Jabir (رضي الله عنه) alonukuliwa akisema: "Baada ya khutba Mtume صلى الله (عليه وسلم) alichinja kondoo kwa mikono yake mwenyewe na huku akisema: Bismillahi, Wallaahu Akbar (kwa jina la Allaah, Mungu ni Mkubwa); hii ni kwa ajili yangu, na kwa ajili ya umma wangu (Waislamu wote) ambao hawakuchinja." Hata hivyo kutokamana na ushahidi huo, hadithi hiyo inapasa kueleweka kama inawahusu tu wale wasokuwa na uwezo. Hii inaonyesha rehema ya Allaah (سبحانه وتعالى). Ambae hakutaka kuwakosesha fadhila na malipo wale wasio na uwezo wa kifedha wa kutekeleza jambo hilo. Pia wameitegemea hadithi ya Umm Salamah (رضي الله عنها) kwenye sehemu ijayo. Hadithi hiyo inaunganisha uchinjaji na kuwa na hiari au nia ya muislamu, ambayo italeta maana ya kuwa na hiari na sio wajib. Hata hivyo mapendekezo hayo hayana nguvu kuupinga ushahidi uliopita. Haswa iwapo mtu atakapoiangalia aya ifuatayo inayofungamanisha jambo la waajib (kufuata njia iliyonyooka) na mapendeleo ya mtu.**"Kwa yule miongoni mwenu anaetaka kushika njia."** [At-Takwir 81:28]

SHURUTI ZA MCHINJAJI

Mapato Ya Halali

Kama ilivyo kuhusu sadaqa nyengine yoyote anayotoa mtu kwa kutaraji radhi ya Allaah (سبحانه وتعالى) inampasa ahakikishe yakwamba mapato yake na zile pesa atakazonunulia kichinjo ni nzuri, au kinyume cha hivyo, Sadaqa haitokubaliwa, kwa sababu, *"Allaah ni Tayyib (mzuri) na hakubali ila kilicho Tayyib (kizuri)..."*

Kujiepusha Kunyoa Nywele Na Kukata Kucha

Yeyote anaekusudia kuchinja (kiongozi wa nyumba) amekatazwa kunyoa au kukata kucha zake kutokea siku ya mwanzo ya Dhul-Hijja mpaka amalizapo kutoa sadaqa (Kuchinja). Umm Salama (رضي الله عنها) akatuhadithia ya kwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Kwa yule alokusudia kuchinja (siku ya 'Idd) basi, pindi mwezi wa Dhul-Hijja uonekanapo, haruhusiwi kunyoa nywele zake (zozote) au kukata kucha mpaka amalize kuchinja."*Na kwenye riwaya nyengine: *"Pindi zitakapoanza siku kumi, kwa wale walonuilia kuchinja,haiwapasi wao kunyoa nywele zao (zozote) au kukata kucha zao (mpaka wamalize kuchinja)."*

Makatazo hayo ndiyo rai ya jamhuri ya wanavyoni wa ma-Salaf (رضي الله عنهم) Inahusika ndani yake kung'oa au kuchoma nwele za kichwa, makwapa, masharubu au nywele zimeazo sehemu za siri.

WAKATI NA MAHALI

IBADA YA KUCHINJA

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

Wakati Wa Kuchinja

Wakati wa kuchinja sadaka unaanza baada ya swala ya 'Idd. Chochote kilochinjwa kabla ya hapo hakiruhusiwi kama Udh-hiyah. Anas (رضي الله عنه) akasimulia ya kwamba Mtume صلى الله عليه (وسلم) amesema: *"Yule alochinja kabla ya swala (ya 'Idd), amechinja (nyama ya kawaida tu) kwa ajili ya nyumba yake na inampasa achinje tena. Ama kwa yule alochinja baada ya swala (ya 'Idd) basi huyo ametekeleza sadaqa yake na amefanya kulingana na Sunna ya Waislamu."*

Vile vile ikapokewa kutoka kwa al-Baraa' (رضي الله عنه) kuwa Mtume صلى الله عليه (وسلم) amesema: *"Kitu cha kwanza tunachofanya siku ya leo (al-Adh-ha) ni kuswali, kisha tunakwenda kuchinja. Kwa yule afanyae hivyo, kwa hakika amefanya kulingana na Sunnah yetu, ama yule aliechinja kabla, basi huyo amejitolea tu nyama kwa jamii yake na wala haihesabiwi kuwa ni (kichinjo cha) sadaqa."*

Wakati huu unaendelea kwenye siku za Tashriq mpaka kutwa kwa jua siku ya tatu baada ya 'Idd ul-Adh-ha. Jubayr Bin Mut'im (رضي الله عنه) akatuhadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Siku zote za Tashriq ni siku za kuchinja."*

Mahali Pa Kuchinja

Imependekezwa kuchinja wanyama katika musalla (viwanja viswaliwavyo swala ya 'Idd) kama alivyofanya Mtume (صلى الله عليه وسلم). Hata hivyo kwa wale wanaotekeleza hajj, wanaruhusiwa kuchinja popote walipo ndani ya Mina, kama alivyosema (صلى الله (عليه وسلم): *"Mimi nimechinja hapa lakini sehemu yote ya Mina ni mahali pa kuchinja, na njia zote za milima ya Makkah (panaruhusiwa) na vichochoro vyake ni sehemu za kuchinja, kwahivyo chinja popote ulipo."*

Wanyama Wanaofaa Kuchinjwa

Kuna aina nyingi ya wanyama wanaofaa kuchinjwa. Mtume Muhammad صلى الله عليه (وسلم) pamoja na maswahaba zake walichinja Ngamia na Ng'ombe (kondoo na mbuzi). Mtume wa Allaah صلى الله عليه (وسلم) aliwahi kuchinja ngamia majike sitini na tatu katika siku ya kuchinja (al-Adh-ha).

Vile vile Mtume (صلى الله عليه وسلم) alichinja Ng'ombe kwa niaba ya wake zake, na akachinja kondoo wawili madume.

Mbuzi Mmoja Kwa Nyumba Moja

Inatosheleza mtu mmoja kuchinja mbuzi mmoja kwa ajili yake na watu wa nyumba yake. Abu Ayyub al-Ansaari aliulizwa kuhusu kuchinja katika wakati wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na akasema: *"Wakati wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) mtu mmoja alikuwa akichinja mbuzi mmoja kwa ajili yake na watu wa nyumba yake. Walikuwa wakila na wakilisha (watu wengine). Baada ya hapo, watu wakaanza kujifakhari (katika vichinjo vyao) kama muonavyo sasa."*

Kushirikiana Katika Wanyama Wakubwa

Jamii za nyumba saba wanaweza kushirikiana kwa Ng'ombe mmoja au Ngamia mmoja. Akasema Mtume صلى الله (عليه وسلم): *"Ng'ombe mmoja anatosheleza watu saba, na Ngamia mmoja anatosheleza watu saba (kama kichinjo)."*

Mnyama Mwenye Afya Nzuri

Kwa vile hili ni jambo la 'ibada na ni sadaqa kwa ajili ya Allaah (سبحانه وتعالى) basi hapana budi mtu atafute mnyama alie bora na awe ni wa kadiri ya uwezo wake. Alikuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) akichagua kwa kichinjo chake, mnyama mzuri asie na kilema chochote.

Wanyama waliobora kuchinja, itakuwa ni kondoo dume mweupe mwenye pembe, awe na alama ya weusi machoni na miguuni. Huu ndio mfano wa mnyama aliekuwa akimpenda Mtume صلى الله عليه (وسلم) na kumchinja.

Kasoro Zisokubalika

Mnyama alokusudiwa kuchinjwa hafai kuwa na kasoro zilizodhahiri zifuatazo: chongo wa jicho moja, mgonjwa, anaechechea, au aliekonda mno.

Ikapokewa hadithi kutoka kwa al-Baraa' Bin Aazib (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: *"Wanyama aina nne hawafai kuchinjwa kwa Udh-hiyah: Yule aliechongo wa jicho moja, yule aliemgonjwa taabani, yule anaechechea na yule aliekonda akadhoofika mifupa yake."*

Pia vile vile Ali (رضي الله عنه) amesema kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuruhusu kuchinja mnyama ambae sikio lake limekatwa kwa mbele, nyuma au katikati.

Wanyama Maksai (Castrated)

Inaruhusiwa kuchinjwa mnyama alovunjwa uzao wake, Abu Raafi' (رضي الله عنه) amesema kuwa Mtume صلى الله عليه (وسلم) alichinja kondoo wawili weupe, madume na waliovunjwa uzao wao.

Umri Wa Wanyama (Vichinjo)

Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiwahimiza maswahaba zake wachinje wanyama walotimia umri mkubwa, lakini pia akawaruhusu kuchinja kondoo wachanga.

'Uqba Bin 'Aamir (رضي الله عنه) akatuhadithia yakwamba Mtume صلى الله (عليه وسلم) aliwagawia maswahaba zake wanyama walochinjwa (baada ya vita) na sehemu yake yeye ikawa ni kondoo mchanga. 'Uqba (رضي الله عنه) akalalamika kuhusu jambo hilo (kwa khofu huwenda nyama ile isikubaliwe kama sadaqa) akasema: "Yaa Rasoolullaah! mimi nilipata kondoo mchanga peke yake." Akamjibu, **"Mtoe Sadaqa!"**

Vile vile Mujaashi' (رضي الله عنه) akatuhadithia kuwa Mtume صلى الله عليه (وسلم) alisema: **"Ruhusa ya kondoo mchanga ni kama mbuzi alokomaa."**

Hadithi hizi pamoja na nyengine zilo sahih zaonyesha mambo yafuatayo kuhusu umri unaoruhusiwa wa wanyama [vichinjo].

[Endelea Katika Makala Yajayo]